*Sauti za Wananchi* *Muhtasari Na. 3* *June 2013*



# Fedha za ruzuku katika shule za msingi:

## Muongo mmoja tangu kuanzishwa, je, fedha zinafika shuleni?





## 1. Utangulizi

Wanafunzi waliofanya mitihani ya Kidato cha Nne mwaka 2012 ni wale walioanza Darasa la Kwanza mwaka 2002. Kwa picha ya haraka, mwaka 2002 ulikuwa mwaka wa kipekee kwa mtu kuanza maisha yake ya shule: ulikuwa ndiyo mwanzo wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), uliokuwa hatua kubwa ya kimaendeleo na ulifungua fursa ya elimu kwa wote, kwani Serikali ilifuta ada katika shule za msingi. Hata hivyo, mwezi Machi 2013, ilibainika waziwazi, kwamba mambo yote yaliishia kwenye kilio kwani zaidi ya nusu ya wanafunzi hao sawa na asilimia 61 ya wanafunzi walipata Daraja la 0. Nini kilitokea?

Waliobuni MMEM waliazimia kwamba kupanua wa elimu ya msingi unapaswa kuendana na kukuza ubora. Hata hivyo, waling'amua kwamba rasilimali zilizokuwa zikifika hadi ngazi ya shule, hasa vitabu, ni kidogo sana. Hivyo chini ya MMEM, ulianzishwa utaratibu wa kisera wa kuzipatia shule ruzuku ya uendeshaji wa shule, itakaotolewa kwa kila mwanafunzi kama nyenzo ya kusaidia kukuza ubora wa elimu. Ruzuku hii ilitolewa sambamba na ruzuku ya maendeleo ambayo ingetumiwa kuboresha au kujenga miundombinuinayostahili katika shule zote za msingi za umma.

Fedha hizi za ruzuku ya uendeshaji kwa kila mwanafunzi zilipangwa kugharimia manunuzi ya vitabu vya kiada na mahitaji mengine ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kukuza ubora wa kujifunza. Ruzuku ya uendeshaji ingeweza pia kutumika kufanya matengenezo madogomadogo, kugharamia shughuli za kiutawala na gharama za mitihani. Ruzuku hii kwa kila mwanafunzi zilipangwa iwe kwa kiwango cha Dola 10 za Marekani (sawa na TZS 16,000 mwaka 2013). Hata hivyo, tangu wakati huo hadi sasa, kiwango hicho kimetafsiriwa kuwa kiasi cha TZS 10,000 katika mipango na bajeti, bila kujali mabadiliko ya thamani ya shilingi ikilinganishwa na dola. Ruzuku hiyo inapaswa kugawiwa mara moja katika kila robo ya mwaka.

Matini hii iliandikwa na kutayarishwa na Uwazi iliyopo Twaweza, ambayo inatumia ofisi ya Hivos Tanzania. Imetolewa mwezi Juni 2013.

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 Nukushi: +255 22 266 4308.
uwazi@twaweza.org www.twaweza.org/sauti

Twaweza
ni sisi

Je, fedha hizi za ruzuku ya uendeshaji wa shule zinafika shule na kwa wakati? Je, walimu na wazazi wanajua kuhusu fedha hizo?

Katika muhtasari huu, Uwazi iliyo Twaweza inawasilisha matokeo kutoka sampuli yenye uwakilishi wa kitaifa wa wahojiwa kutoka kote Tanzania Bara. Takwimu hizi zimekusanywa na *Sauti za Wananchi*, mradi wa utafiti kwa njia ya simu za mkononi nchini Tanzania na wa kwanza wa aina yake barani Afrika. Matokeo yaliyo katika muhtasari huu yamejikita katika duru la pili la *Sauti za Wananchi*. Simu zilipigwa kati ya tarehe 11 na 25 Aprili, 2013; data hizi zinajumuisha majibu kutoka kaya 1,762 na walimu wakuu 112. Matokeo muhimu ya muhtasari huu ni:

- Asilimia 34 ya shule za msingi hazikupokea fedha zozote za ruzuku ya uendeshaji kwa mwaka 2013 hadi kufika tarehe 25 Aprili, 2013
- Wastani wa kiasi cha fedha iliyotolewa na Serikali mwaka 2013 ulikuwa TZS 2,094
- Wastani wa fedha zilizopokelewa kati ya 2010 na 2012 ni TZS 2,202 kwa mwanafunzi
- Asilimia 93 ya walimu wakuu walitaarifu kutopokea vitabu vya kiada kwa idadi ya kutosheleza.


# 2. Mambo makuu saba kuhusu Ruzuku ya Uendeshaji wa Shule nchini Tanzania

## Jambo la 1: Wazazi walio wengi hawajui kuhusu fedha za ruzuku

Walimu, wanafunzi na wazazi ndiyo wanaotarajiwa kunufaika na sera ya fedha za ruzuku na kwa hiyo wana kichocheo kikubwa zaidi cha kufuatilia kama fedha zinafika na kama zinafika katika kiwango cha kutosha. *Mradi wa Sauti za Wananchi* uliwahoji wazazi – wenye watoto wanaosoma shule ya msingi hivi sasa au waliotoka shule ya msingi ndani ya miaka miwili iliyopita – kama wamewahi kusikia kuhusu fedha za ruzuku kwa kila mwanafunzi.

Jibu ni hasi kwa asilimia 79 ya wazazi (Kielelezo cha 1). Hata hivyo utafiti huu umegundua kwamba kuna tofauti ndogo ya uelewa kuhusu fedha hizi za ruzuku kati ya wahojiwa wa vijijini na wale wa mjini, au kati ya wahojiwa masikini na wasio masikini (umasikini hapa unabainishwa kwa umiliki mali, kaya maskini ni kundi la chini la asilimia 40 kwa maana ya mali wanazomiliki). Hii ina maana kwamba wananchi hawawezi kufuatilia, achilia mbali kudai, ruzuku hii ya msingi lakini iliyo muhimu kwani ina athari ya moja kwa moja katika ubora wa elimu ya watoto wao.


**Kielelezo cha 1: Umewahi kusikia kuhusu ruzuku kwa kila mwanafunzi?**




**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu za Mkononi – Awamu ya 2, Aprili 2013.

Walimu wakuu walipoulizwa kuhusu kiasi cha ruzuku kwa kila mwanafunzi, asilimia 54 waliweza kubaini kiasi kilichotajwa katika mipango ya sasa, yaani TZS 10,000 (Kielelezo cha 2).

**Kielelezo cha 2: Je, walimu wakuu wanajua kuhusu kiasi cha ruzuku kwa kila mwanafunzi?**





**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu za Mkononi – Awamu ya 2, Aprili 2013.

## Jambo la 2: Asilimia 34 ya shule za msingi hazijapokea ruzuku kabisa

Kielelezo cha 3 kinaonyesha kiasi cha fedha za ruzuku kwa kila mwanafunzi kilichopokelewa shuleni kama ilivyotolewa taarifa na walimu wakuu wakati wa kupiga simu, yaani, kwa kipindi kabla ya tarehe 25 Aprili 2013. Katika asilimia 34 ya shule, walimu wakuu walionyesha kwamba hawakuwa wamepokea fedha za ruzuku kwa mwaka 2013. Wastani wa ruzuku hiyo kwa mwaka 2013 ulikuwa TZS 3,094.


**Kielelezo cha 3: Je, shule yako ilipokea fedha za ruzuku kiasi gani kwa mwaka 2013?**




**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu za Mkononi – Awamu ya 2, Aprili 2013.

Data kutoka kwenye awamu hii ya utafiti kwa simu za mkononi na utafiti wa msingi wa mradi wa *Sauti za Wananchi* zinaonyesha kwamba wastani wa mwaka wa fedha za ruzuku kwa kila mwanafunzi zilizopokelewa ni TZS 5,000 tangu mwaka 2010 (Kielelezo cha 4, data ni kwa shule zilizopigiwa simu tu katika awamu hii). Wastani kwa miaka yote minne ni TZS 2,202 kwa mwanafunzi.

**Kielelezo cha 4: Wastani wa fedha za ruzuku zilizopokelewa 2010—2013**




**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti wa Msingi na ule wa Simu – Awamu ya 2, Aprili 2013

Hadi mwisho wa robo ya kwanza ya 2013, wastani wa asilimia 20 wa fedha za ruzuku zilipokelewa shuleni. Kama Serikali Kuu na Serikali za mitaa zingelitoa fedha hizi za ruzuku kwa kila robo ya mwaka 2013, jumla ya ruzuku kwa kila mwanafunzi ingekuwa TZS 8,000. Ingelikuwa hivyo, kiasi hiki kingekuwa bado cha chini ikilinganishwa na kilichostahili yaani Tsh. 10,000. Hata hivyo kiasi hiki kingelikuwa cha juu kuliko ilivyokuwa katika miaka miwili iliyopita. *Sauti za Wananchi* itaendelea kufuatilia upokeaji wa fedha za ruzuku kila baada ya muda fulani na kutoa taarifa.


## Jambo la 3: Walimu wakuu wana mwongozo wa matumizi ya ruzuku ya uendeshaji na wanaweka taarifa ya matumizi kwenye mbao za matangazo

Fedha za ruzuku zinatolewa na serikali kwa kutokana na bajeti ya mwaka husika. Ili kuhakikisha uwazi na uwajibikaji wa matumizi ya fedha hizi, Serikali ilitoa mwongozo rasmi kwa ajili ya kutoa maelekezo ya matumizi ya fedha za ruzuku kwa kila mwanafunzi. Idadi kubwa ya walimu wakuu (95%) walitoa taarifa kwamba shule zao zina mwongozo huo.

Walimu wakuu walipoulizwa kuhusu asilimia ya fedha za ruzuku inayopaswa kutumiwa kununulia vitabu kwa mujibu wa mwongozo, asilimia 86 ya walimu wakuu walitoa jibu lililooana na maelekezo ya Wizara ya Elimu kwamba asilimia 40 ya fedha hizo za ruzuku itengwe kwa ajili ya kununulia vitabu. Maelekezo zaidi ni kwamba taarifa ya matumizi ya fedha za ruzuku lazima ibandikwe kwenye mbao za matangazo shuleni. Idadi kubwa ya walimu wakuu (80%) walitoa taarifa kwamba wanafuata mwongozo huo (Kielelezo cha 5).

Tafsiri moja ya matokeo haya ni kwamba katika ngazi ya shule hakuonekani kuwepo kwa changamoto kubwa katika utekelezaji wa sera ya fedha za ruzuku: mwongozo upo na ni dhahiri, kutokana na majibu ya walimu wakuu kwamba mwongozo huo unaeleweka vizuri. Kwa maneno mengine, taratibu za kupokea fedha za ruzuku na matumizi yake zipo katika shule.

**Kielelezo cha 5: Je, taarifa za matumizi ya fedha za ruzuku zinawekwa wapi kwa ajili ya hadhira kuona?**





**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu za Mkononi – Awamu ya 2, Aprili 2013.

## Jambo la 4: Shule hutumia fedha za ruzuku kwa mujibu wa kanuni

MMEM inaeleza kwamba fedha za ruzuku zinapaswa kutumika kulipia vitabu, zana za kujifunzia, kukarabati suhula, vifaa vya ofisi; na pia kulipia gharama za uendeshaji kama vile uandaaji wa mitihani n.k. Pale *Sauti za Wananchi* ilipowauliza walimu wakuu kuhusu namna wanavyotumia fedha za ruzuku, walio wengi walijibu kama maelekezo ya sera yanavyoainisha (Kielelezo cha 6).

**Kielelezo cha 6: Walimu Wakuu waliripoti kuhusu namna wanavyotumia fedha za ruzuku**





**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu za Mkononi – Awamu ya 2, Aprili 2013.

## Jambo la 5: Asilimia 93 ya walimu wakuu walikiri kuwa na upungufu wa vitabu

Walipoulizwa kuhusu kununua vitabu, asilimia 87 ya walimu wakuu walitoa taarifa kwamba wamenunua vitabu vichache tu tangu mwaka 2010. Manunuzi hayo kwa kiasi kikubwa yalifanywa kwa fedha za ruzuku. Ni asilimia 14 tu ya walimu wakuu waliafifu kununua vitabu kwa kutumia fedha za vyanzo vingine. Mifano ni manunuzi kwa kutumia michango ya jamii na wazazi; kutumia fedha shule inazopata kutokana na kazi za kilimo; misaada

kutoka makampuni; na misaada kutoka asasi za kiraia. Walipoulizwa endapo hivi sasa shule inapokea vitabu inavyohitaji kwa kiwango cha kutosha, asilimia 93 ya walimu wakuu walisema hapana (Kielelezo cha 7). Matokeo haya yanaungwa mkono na majibu kutoka kwa wazazi: asilimia 55 ya wazazi wenye watoto katika shule za msingi waliripoti kwamba watoto wao hawana vitabu vya kiada kabisa (tazama *Sauti za Wananchi* Muhtasari wa 1, Mei 2013).

**Kielelezo cha 7: Je, shule kwa sasa inapokea vitabu inavyohitaji kwa idadi inayotosheleza?**





**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu za Mkononi – Awamu ya 2, Aprili 2013.

## Jambo la 6: Wazazi wanaendelea kutoa michango katika shule za msingi za umma

Lengo la msingi la fedha za ruzuku lilikuwa kufidia mapato ya shule yaliyopotea baada ya ada kufutwa chini ya MMEM, kwa madhumuni ya kuhakikisha upatikanaji wa elimu wenye ubora kwa wote. Hata hivyo, walipoulizwa kama wanatoa michango yoyote ya kifedha shuleni kwa ajili ya watoto wao kuhudhuria masomo, asilimia 87 ya wazazi walitoa taarifa kwamba wanafanya hivyo. Kielelezo cha 9 kinatoa mgawanyo wa majibu kuonyesha aina ya michango wanayotoa wazazi; kila mhimili unatoa asilimia ya jumla ya majibu ya ndiyo yaliyotolewa.

**Kielelezo cha 8: Aina za michango iliyolipwa na wazazi**





**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu za Mkononi – Awamu ya 2, Aprili 2013.

## Jambo la 7: Walimu wakuu hawaridhishwi na jinsi fedha za ruzuku inavyotolewa

Walimu wakuu wanahusika na uendeshaji wa shule wa siku hadi siku na kwa hiyo wanategemea sana fedha za ruzuku. Walimu wakuu walipoulizwa kuhusu kama wanaridhishwa na jinsi fedha za ruzuku inavyotolewa, asilimia 63 walieleza kutoridhishwa, asilimia 28 hawakuwa na maoni, na asilimia 9 tu ndiyo walioeleza kuwa wanaridhika.


**Kielelezo cha 9: Walimu wakuu walieleza kutoridhishwa na utoaji wa fedha za ruzuku**




**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu za Mkononi – Awamu ya 2, Aprili 2013.

Walimu wakuu walipoulizwa njia gani walikuwa wanazitumia kufuatilia fedha za ruzuku, makundi ya majibu katika Kielelezo cha 11 ndiyo yaliyotolewa. Majibu yaliyo mengi (39%) yanaonyesha kwamba walifanya mawasiliano na Ofisi ya Elimu wa Wilaya; hii pia inaonyesha kwamba walimu wakuu wanaelewa namna mfumo unavyofanya kazi kwa kuwa fedha za ruzuku zinatumwa kupitia ofisi za Halmashauri. Asilimia 17 waliripoti kutofuatilia.

**Kielelezo cha 10: Je, walimu wakuu wanafuatilia wapi utolewaji wa fedha za ruzuku?**




**Chanzo cha data:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa Simu za Mkononi – Awamu ya 2, Aprili 2013.

# 3. Hitimisho

Muhtasari huu unatoa matokeo mbalimbali kuhusu ruzuku ya uendeshaji wa shule kwa kutumia mahojiano na wazazi na walimu wakuu kutoka kote Tanzania Bara. Matokeo makuu yana sura tofauti: Kati ya Januari na Aprili 2013, shule nyingi zilikuwa bado hazijapokea fedha zozote. Kwa upande mwingine, hadi Aprili 25 2013, shule zilikuwa zimeshapokea wastani wa fedha zilizotolewa kwa mwaka kati ya 2010 na 2012. Je, utoaji fedha za ruzuku kwa mwaka 2013 utakuwa wa haraka zaidi kuliko miaka ya nyuma na kufikia kiasi kamili cha TZS 10,000 kwa kila mwanafunzi? Utafiti wa *Sauti za Wananchi* utakaofuatilia utoaji wa ruzuku hii kwa kipindi kijacho utatupatia majibu.

Kutokana na utafiti huu, ni dhahiri kwamba kwa upande wa shule, taratibu za matumizi ya fedha za ruzuku ziko kwani shule zina mwongozo na unaeleweka; fedha zinazopokelewa zinasemekana kutumiwa kugharamia mahitaji yaliyoainishwa; na taarifa za matumizi zinawekwa kwenye mbao za matangazo kwa ajili ya kuwaarifa wanaotaka kujua, wakiwemo wazazi. Hata hivyo, kama fedha hazipatikani, muundo huu hauwezi kutumiwa kukuza ubora wa kujifunza, na walimu, wazazi na jamii wanaweza kukatishwa tamaa na kuacha kufuatilia jambo hili.

Kwa kuwa Serikali imeshindwa kutoa ruzuku kwa viwango kamili na kwa muda katika miaka ya hivi karibuni, haishangazi kwamba karibu walimu wakuu wote waliripoti kuwa na vitabu vichache tu vya kiada, matokeo ambayo pia yalitajwa na wazazi. Hali hii inatofautiana sana na hali ya shauku na matumaini iliyokuwepo wakati wa kuanzishwa kwa MMEM mwaka 2001, ambapo lengo lililokuwa limewekwa kufikia lengo la kuwa na kitabu kimoja kwa mwanafunzi ifikapo mwaka 2006.

Sio vigumu kuona kwamba kuna uhusiano kati ya kutotimizwa kwa malengo ya MMEM na matokeo mabaya ya mitihani ya Kidato cha Nne mwaka 2012, kwa kundi lile lile lililoanza safari ya elimu wakati (Darasa la 1-7, Kidato cha 1-4) MMEM ilipoanza mwaka 2002. “Kizazi hiki cha kielimu kilichopotea” kinaibua maswali makubwa kuhusu menejimenti na usimamizi wa MMEM na watendaji wanaohusika, wakiwamo dhima za Bunge na jumuiya ya wahisani. Suala kubwa linaloibuliwa hapa ni uwazi kuhusu bajeti ya umma: je, fedha hazikufika shuleni kwa sababu kulikuwa na ukosefu wa fedha au kwa sababu ya uwekaji kipaumbele mbovu na kukosekana kwa uwazi?

Njia moja yenye nguvu inayoweza kutumiwa kujibu maswali haya ni kutekeleza ahadi ya Tanzania ya uwekaji wazi data chini ya Ushirikano wa Serikali Wazi *(‘Open Government Partnership’*), ambayo imepata msukumo mpya kupitia mradi wa ‘*Big Results Now’*. Chini ya sera ya data wazi, mtu yeyote – wakiwamo wazazi, walimu, maofisa elimu, wakaguzi wa hesabu, wabunge na Rais – wanapaswa kuweza kutumia tarakilishi au simu ya mkononi kujua nini kinaendelea katika kila shule, wilaya na nchi. Inapaswa kuonyesha idadi ya wanafunzi, kiasi cha fedha (za ruzuku) zilizotengwa katika bajeti na kutolewa kwa mwaka huo, na tarehe fedha hizo zilipotolewa, na pia taarifa nyingine nyingi zinazostahili katika ngazi ya shule. Taarifa hizi za kiutawala ziripotiwe kila mwaka na walimu wakuu na kukusanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kwamba kile kinachohitajika ni kuzinasa na kuzifanya ziwe hadharani. Serikali ingeweza kutoa fursa au wananchi kutoa mrejesho sambamba na data rasmi, ili kwamba wale wanaohusika waweze mara moja kuchukua hatua. Upatikanaji wa haraka wa data kama hizo utasaidia kubaini upungufu na unaweza kuondoa hali ya sasa ya upungufu wa vitabu na zana za kujifunzia. Zaidi ya hayo, jukwaa kama hilo lingeweza kujenga imani ya umma na kuiamini serikali, na kutoa mchango katika kutatua migogoro ya kujifunza inayoikabili Tanzania.